
Jumatano Desemba 17, 2025

**Nukuu**



Ni vizuri kufurahia mafanikio lakini ni n

**Bill Gates- Mwanzilishi wa Microsoft**

# Kanuni mpya za madereva zijadiliwe kwa kina

Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) imeanza mchakato wa kutunga kanuni zitakazosimamia suala la uchovu wa madereva wa magari ya biashara, hatua ambayo tunaipongeza, tukiweka angalizo la wadau kuzijadili kwa kina kabla ya kutoa baraka zao.

Dhamira ya kanuni hizo ni njema, hasa ikizingatiwa kuwa uchovu ni miongoni mwa vyanzo vikuu vya ajali nchini, hata hivyo, ni muhimu kanuni hizi zikajadiliwa kwa utulivu na wadau ili ziwe zinatekelezeka, badala ya kuibua manung'uniko na misuguano.

Tunasema hivyo kwa sababu bila wadau kujadili rasimu ya kanuni zinazopendekezwa kwa hoja na bila mihemuko, tunaona Serikali kupitia Latra inaweza kutunga kanuni zisizo shirikishi, ambazo utekelezaji wake unaweza kuwa mgumu.

Mathalani, kuna kanuni zilizotungwa mwaka 2010 na kufanyiwa marekebisho mwaka 2017 kwa ajili ya kusimamia leseni za usafiri wa bajaji za kukodi. Hata hivyo, tunaona katika maeneo mengi nchini bajaji zinaendeshwa kinyume chake, mithili ya daladala.

Hali hii ya kutosimamiwa ipasavyo kwa masharti ya kanuni za leseni za bajaji za biashara, imeibua msuguano ya kila mara kati ya wamiliki na madereva wa daladala kwa upande mmoja, na mamlaka za usimamizi kama Latra na askari wa Usalama Barabarani kwa upande mwingine.

Kanuni hizo zinataka dereva wa bajaji awe na leseni halali ya udereva, chombo anachoendesha kiwe na bima, na kisibebe zaidi ya abiria watatu pamoja na dereva. Tujiulize leo hali ilivyo barabarani kwetu kuhusu usafiri wa bajaji ni ipi?

Ni kwa msingi huo ndipo tunaposema ni muhimu katika kikao cha kujadili rasimu ya kanuni zitakazosimamia uchovu wa madereva kitakachofanyika Desemba 22, 2025, wadau washirikishwe kikamilifu na maoni yao yazingatiwe kadri inavyowezekana.

Wadau tunaowazungumzia hapa ni pamoja na madereva wenyewe ambao kanuni hizi zimewalenga, wakiwamo wa mabasi; wamiliki ambao ndio huwalipa madereva mishahara na posho; kampuni za bima; pamoja na vyama vya wafanyakazi.

Mathalan, rasimu ya nanuni hizo inaweka wazi viwango vya saa za kuendesha gari kwa siku na kwa wiki, pamoja na mapumziko ya lazima kama sehemu ya mkakati mpana wa usalama katika usafiri wa umma wa kibiashara.

Kwa mujibu wa kanuni zinazopendekezwa, dereva hataruhusiwa kuendesha gari la huduma ya umma kwa zaidi ya saa tisa ndani ya kipindi cha saa 24, wala kuzidi saa 48 za kuendesha ndani ya siku saba za wiki.

Chini ya kanuni hizo, zitakapopitishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali (GN), dereva hataruhusiwa kuendesha zaidi ya saa tano mfululizo bila kuchukua mapumziko. Hapo kuna ulazima wa kuwashirikisha madereva na waajiri wao katika kutoa maoni, ili kanuni zitakapokuwa sheria ziweze kutekelezeka. Kwa kupunguza saa za kuendesha gari, maana yake kutahitajika kuajiri madereva zaidi.

Kwa hiyo, wakati wa kujadili kanuni hizo, ni muhimu kuzingatia kuwa zinaweza kuongeza gharama za uendeshaji kwa wamiliki wa mabasi au magari ya biashara. Je, wana uwezo huo? Kama hawana, kanuni hizo zisomekeje au zitaathiri masuala ya upangaji wa nauli?

Utaratibu kama huo unatumika katika ndege za kibiashara, ambapo kwa ndege yenye rubani mmoja, muda wa juu wa rubani kuendesha ni saa nane ndani ya saa 24, na kwa ndege yenye marubani wawili ni saa 10. Tukitaka iwe hivyo pia kwa mabasi na daladala lazima tujadili kwa kina bila mihemuko ili kanuni ziweze kutekelezeka.

## KIPANYA




MWANANCHI COMMUNICATIONS LTD

**HUTOLEWA NA MWANANCHI COMMUNICATIONS LIMITED (MCL)**

Barabara ya Mandela, SLP 19754, Dar es Salaam
+255 22 24 50875, 0754 780647, 0765 864917
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Rosalynn Mndolwa-Mworia:** Mkurugenzi Mtendaji
**Mpoki Thompson:** Mhariri Mtendaji Mkuu
**Joseph Damas:** Mhariri Mtendaji

*Tunawezesha taifa*

Daily News Desemba 17, 2025 Pg 6.




***DEPUTY Minister for Transport, David Kihenzile is briefed by Director General of Land Transport Regulatory Authority( LATRA), Dr Habibu Suluo when he visited the authority's booth during the 18th Transport Sector Performance Review Meeting Exhibition, where he observed various regulatory activities implemented by the Authority in Arusha, yesterday.(Photo by a Correspondent)***

CamScanner

## TAHARIRI

HabariLEO

# 'Mchezo mchafu' usafiri wa mabasi usifumbiwe macho

KATIKA kipindi hiki cha mwisho wa mwaka, kumekuwapo na ongezeko kubwa la wasafiri wa masafa marefu, hasa kwa mabasi wakienda kusherehekea sikukuu za Krisimasi na Mwaka Mpya.

Ni kipindi ambacho mahitaji ya vyombo vya usafiri huongezeka kiasi cha mamlaka kutoa usajili wa muda wa vibali vya usafirishaji kwa watu wanaotaka kufanya hivyo kwa kuweka vigezo.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) huchukua hatua za kutoa leseni za muda mfupi kwa mabasi ili kuongeza huduma katika njia zenye mahitaji makubwa kipindi cha sikukuu na kupunguza msongamano wa usafiri

Vilevile, hiki ni kipindi ambacho huwapo changamoto ambazo hurudisha nyuma jitihada za kuboresha usafiri nchini.

Moja ya changamoto hizo ni ulanguzi wa tiketi, matapeli na biashara haramu ya tiketi, ambayo husababisha wasafiri kushindwa kupata huduma kwa haki na wakati muafaka.

Mathalani, katika gazeti hili jana kulikuwa na habari kuhusu wakala wa basi la kampuni moja anayetafutwa na Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani wilayani Kahama akituhumiwa kumtoza abiria Sh 135,000 kinyume cha sheria.

Aidha, inapofika tarehe za karibu na Krisimasi, vitendo vya ulanguzi wa tiketi katika Kituo cha mabasi cha Magufuli Dar es Salaam, huripotiwa wakidaiwa kuuza tiketi za karatasi kwa gharama kubwa kwa wasafiri wanaokwenda mikoa mbalimbali.

Huu ni mchezo mchafu ambao watu wasio waaminifu hukandamiza haki za wasafiri na wakati huo huo kuipotezea serikali mapato.

Hata hivyo, tunapongeza mamlaka mbalimbali za serikali ambavyo hufanya kazi ya ziada kusimamia usafirishaji huu wa umma katika kipindi hiki cha sikukuu.

Rai yetu kwa serikali ni kuongeza jitihada za kusimamia mfumo wa tiketi mtandao unaolenga kuhakikisha tiketi zinapatikana kwa njia rasmi na salama.

Mfumo huu wa mtandao unatoa uwazi zaidi, unafanya tarifa za wasafiri kuwa rahisi, na hupunguza fursa za ulanguzi na ulaghai unaohusiana na tiketi za mabasi.

Kwa upande wa wasafiri, wanapaswa kuelewa kuwa kununua tiketi kwa njia rasmi kunawalinda dhidi ya udanganyifu wa tiketi za karatasi zinazouzwa kwa bei ya juu na wakati mwingine zinaweza kuwa bandia.

Wananchi hawana budi kutambua kwamba tiketi za mtandaoni ni muarobaini wa utapeli na matapeli.

Ni matumaini yetu kwamba serikali itaendeleza mikakati ya kudhibiti 'mchezo mchafu' katika usafiri wa mabasi kwa kushirikisha wadau mbalimbali na zaidi kwa kuendelea kuelimisha wananchi juu ya mifumo ya tiketi mtandao.

Wakati huo huo, wananchi na wasafiri wanapaswa kushirikiana kikamilifu na juhudi hizi za serikali kwa kununua tiketi kwa njia rasmi na kutumia teknolojia inayoelekeza matumizi ya mtandao badala ya kutegemea wapigadebe wasio waaminifu.

Kwa kufanya hivyo, usalama wa usafiri utaongezeka, udanganyifu utapungua kama si kukoma na kuhakikisha kila msafiri anapata huduma bora na salama, hasa wakati huu wimbi la wasafiri kuelekea sikukuu.

tsn TANZANIA STANDARD NEWSPAPERS

| | | |
|---|---|---|
| Kaimu Mhariri: | Mgaya Kingoba | 0754-585568 |
| Mhariri wa Habari | Basil Msongo | 0713-761006 |
| Mhariri wa Habari Msaidizi: | Maulid Ahmed | 0735-296549 |
| Mhariri wa Makala: | Joseph Sabinus | 0788 007070 |
| Mhariri wa Michezo: | Clecence Kunambi | 0714 912081 |
| Kaimu Mhariri Msanifu Mkuu: | Stella Nyemenohi | 0713 525127 |

TSN MEDIA GROUP

| | |
|---|---|
| Mkurugenzi Mtendaji: Asha Dachi | 0786-467133 |
| Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara: Soter Salema | 0765-288798 |
| Meneja Mauzo na Usambazaji: Jonathan Manhe | 0653-912475 |
| Meneja Masoko na Utangazaji wa Bidhaa: Felix Mushi | 0754-492310 |
| Meneja Standard Printers: Selemani Mwaitenga | 0745-599029 |

Hotline + 255 286 4862, Simu: 255 286 4864, 255 286 4871
Fax: +255 286 4868 E-mail: mhariri@tsn.go.tz

CamScanner

TAHARIRI

# Kanuni kwa uchovu wa madereva ni mwafaka

HATIMAYE baada ya kurejesha usafirishaji nyakati za usiku nchini, Serikali sasa inakuja na kanuni zitakazobana madereva wa mabasi na malori ya mizigo, ili kukabiliana na ajali barabarani.

Kanuni hizo zinazotarajiwa kuwekwa hadharani rasmi kwenye mkutano uliopangwa kufanyika Desemba 22 mwaka huu, baina ya wadau na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), zinalenga kuwapangia madereva muda wa kazi.

Hiyo ni kutokana na baadhi ya madereva kuendesha magari yao usiku bila kupumzika na hatimaye kujikuta wanashikwa usingizi, lakini wengine kuugua na kujikuta wakisababisha ajali zinazogharimu maisha na mali.

Kanuni hizo kama zitapita basi zitataka kuwapa mapumziko ya lazima kwa madereva, angalau ya saa 10 katika kila saa 24 za kazi, yaani mapumziko ya dakika 30 baada ya kila saa tano za kuendesha mfululizo na saa 24 ndani ya siku saba za kazi.

Tunaungana na wadau kuipongeza Serikali kupitia LATRA, kwa kuja na wazo hilo, litakalosaidia kuepusha ajali zisizo za lazima, ambazo zimekuwa zikipora roho za Watanzania lakini pia kusababisha uharibifu na upotevu wa mali.

Ni jambo la kutia moyo hata hivyo, kwamba kuna baadhi ya wamiliki wa magari tayari walishaanza utaratibu huo, baada ya kubaini kiini cha ajali zinazotokea kila mara, na hivyo wakalazimika kuajiri madereva zaidi.

Hivyo pamoja na kuongeza gharama ya kuajiri madereva wengi, lakini inasaidia kuepusha kadhia hiyo ya ajali na kufanya abiria wengi waamini usafiri na usafirishaji huo wa usiku, ambao hivi sasa umevutia wengi.

Hata hivyo, bado pia kuna ugonjwa sugu wa rushwa kwa baadhi ya askari wa usalama barabarani wasio waaminifu, ambao wamekuwa wakiendekeza vitendo hivyo kwa maslahi yao binafsi na kuchochea ajali.

Tunashauri wakati kanuni hizo zitakapojadiliwa na kukubaliwa katika mkutano wa Desemba 22, itafutwe njia mwafaka ya kugundua nani hatazingatia na kuzifuata, lakini pia jinsi ya kukabiliana na polisi waovu wa usalama barabarani.

Kwa vyo vyote vile, safari bila ajali inawezekana endapo sote watumiaji wa barabara na vyombo vya moto tutakuwa makini na kusaidiana kupambana na wanaokiuka sheria na kanuni zilizopo, hivyo ni vema LATRA ikasisitiza mawasiliano na abiria.

Kufanya hivyo, kutawezesha abiria kuwasiliana na maofisa wa LATRA pale ambapo watabaini madereva na wadau wengine hawashiriki kuepusha ajali barabarani, na hatua kuchukuliwa sawia kwa maslahi mapana ya Taifa.

**BODI YA UHARIRI**

| | |
|---|---|
| **Mwenyekiti** Mbaraka Islam | - +255 755 888819 |
| **Ofisa Mtendaji Mkuu** Salim Abdallah | - +255 713 146553 |
| **Kaimu Mhariri Mkuu** Anicetus Mwesa | - +255 712 727244 |
| **Idara ya Masoko/Matangazo** Aluw Amar | - +255 752 101020 |

Gazeti hili hutolewa na Raia Mpya Limited, kupigwa chapa na Mwananchi Communications Limited. SIMU: +255 733 909090, Idara ya Biashara: 0733 909090, Email: raiatz@gmail.com, S.L.P 11079, Dar es Salaam. Jengo la NHC, Ex Nedco ghorofa ya pili, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi. Tovuti:www.raiamwema.com

CamScanner

# Polisi yaonya ulanguzi tiketi za mabasi

**Na Yohana Shida, Geita**

JESHI la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani limekemea tabia ya mawakala wa mabasi ya abiria kufanya ulanguzi wa tiketi ikisema itawachukuliwa hatua.

Ofisa Mnadhimu Makao Makuu ya Kikosi cha Usalama Barabarani, Butusyo Mwambelo alitoa karipio hilo baada ya ukaguzi wa vyombo vya usafiri katika kituo cha mabasi mjini Geita.

Mwambelo alisema mbali na mahitaji makubwa ya usafiri kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka, maofisa usafirishaji wanapaswa kusimamia miongozo yote ya gharama na sheria za usafirishaji.

"Wajibu wa kondakta ni kuhakikisha watu hawaondoki stendi, kuhakikisha kila mtu ana tiketi, inayoendana na fedha aliyotoa pamoja na nauli inayoendana na maelekezo ya LATRA (Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini)," alisema Mwambelo.

Aliongeza: "Mawakala mmezidi, mwisho wa mwaka tufanye kazi tukiwa na hofu ya Mungu, kwa sababu mawakala mnachukua tiketi zote za mtandaoni gari zima au nusu ya gari."

Alisema wamebaini kuwa baadhi ya mawakala na makondakta wa mabasi ya mikoani wanalangua tiketi na kuziuza kwa bei ya juu hali inayoashiria utapeli kwa abiria.

"Mtu anaenda kutafuta tiketi ya safari, anaambiwa gari limejaa, au anaambiwa kuna siti moja imebaki, kwa sababu ana shida anachukua hiyo tiketi kwa gharama ya juu," alifafanua.

Alitaja changamoto nyingine ya tiketi zilizolanguliwa ni kukosa taarifa sahihi za abiria, hivyo inapotokea ajali mara nyingi tiketi hizo zinakuwa na majina tofauti na abiria halisi.

Aliagiza viongozi wa mawakala wa vituo vya mabasi nchini kuhakikisha wanakomesha tabia ya ulevi kwa mawakala wa mabasi kwani ndio chanzo cha utapeli na wizi.

Kaimu Ofisa Usalama wa Barabarani mkoani Geita, Lazaro Masembo alisema ufuatiliaji unaendelea kudhibiti makondakta na madereva wote wanaojihusisha na kutapeli abiria ndani na nje ya vituo vya mabasi.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) mkoani Geita, Rajabu Selemani alisema milango ipo wazi kwa abiria wote kutoa taarifa wanapohisi kutapeliwa safarini.

Alisema Latra inatekeleza wajibu wake na inafanyia kazi kwa wakati taarifa zote zinazotolewa na abiria ama wadau wa usafiri ili kukomesha tabia ya utapeli kwa maofisa usafirishaji.

CamScanner